# HERI WALIO MASKINI WA ROHO MAANA UFALME WA MBINGUNI NI WAO.
# Math 5: 3, Isaya 57: 15, Zab 34: 18

I. **UTANGULIZI**

Yesu alianza hotuba yake ya mlimani kwa kuwafundisha wanafunzi wake siri ya kuzipata Baraka halisi za Mungu katika maisha yao.

- **Baraka za Mungu zikiwa pamoja na wanafunzi wa Yesu, kamwe haziwezi kulinganishwa na mafanikio binafsi ya vitu vya dunia hii alivyonavyo.**
- Tunasema kwamba Yusufu alifanikiwa sana (alibarikiwa sana), siyo kwamba hakupitia katika mateso mengi na taabu nyingi laa hasha; bali popote alipokwenda, Bwana alikuwa pamoja naye, alitenda kazi pamoja naye na wakati wote alimpa msaada na uwezo (maarifa) ya kuvuka katika kikwazo fulani kilichojitokeza mbele yake. ***Mwz 39: 1 – 6, Mwz 39: 7 – 12, 13 – 23, 40: 1 – 22, 41: 1 – 46 n.k***
- Mwanafunzi aliye na Baraka ya Mungu siyo kwamba hapati dhiki na majaribu mengi, bali daima katika yote anayokutana nayo, Bwana anakuwepo kumwezesha na kumtia nguvu ili aweze kustahimili na hatimaye kuvuka kwa kishindo kikubwa kinachompa Mungu utukufu mkubwa. ***Ufun 2: 8 – 10***

II. Yesu alianza kuwafundisha wanafunzi wake kwa kuwaaambia **"Heri walio maskini wa roho maana ufalme wa Mbinguni ni wao. *Math 5: 3"***

- Hii ni **Heri** ya kwanza iliyo muhimu sana na ambayo ndiyo inayobeba heri nyingine **nane** zote zinazofuata baadae; **kuwa maskini wa roho maana yake halisi ni pale mwanafunzi wa Yesu anapoishi katika wokovu kwa kujitambua daima kwamba yeye kama yeye hana uwezo wa kujitosheleza kiroho; bali kila wakati anamhitaji Mungu na nguvu zake pamoja na neema yake kumsaidia na kumshikilia siku zote hadi atakapo urithi ufalme wa Mbinguni."**

- Yesu baadae alifafanua heri hii kwa uwazi zaidi pale alipowaambia wanafunzi wake kwamba yeye ndiye mzabibu wa kweli na wanafunzi wake ni matawi tu ya huo mzabibu. ***Yoh 15: 1 – 8.***
- **Ni pale tu tawi linapokuwa limeendelea kuunganishwa na shina ndipo linapokuwa hai na baadae kuzaa sana, na kila mwanafunzi atakayeendelea kuunganishwa na Yesu Kristo kama chanzo cha uhai wake kiroho, ndiye atakayezaa sana.**
- Isaka ni mojawapo wa watumishi wa Mungu waliokuwa na heri hii ya kuwa maskini wa roho!! Yeye alijitambua daima kwamba hana uwezo wa kujitosheleza kiroho, na wakati wake wote wa maisha yake alimhitaji Mungu na nguvu zake na neema zake kumsaidia na kumvusha katika hatari nyingi alizokuwa anakabiliana nazo akiwa katika Nchi ya kigeni. ***Mwanzo 26: 1 – 33. * mst 2, 12, 24.***
- Pale mwanafunzi anapodumu kukaa ndani ya Yesu yaani pale anapokuwa na muda wa kuishi karibu na Yesu Kristo kwa njia ya kujifunza na kutafakari Neno lake, ndivyo maombi yake yanavyozidi kuwa sawasawa na yenye kufanikiwa sana; hii ndiyo maana ya kuwa maskini wa roho; **yaani kila wakati unadumisha tabia ya kuwa karibu na Bwana Yesu kwa lengo la kupokea nguvu zitakazokuwezesha kukabiliana na kila aina ya changamoto zitakazojitokeza mbele yako bila kuzimia moyo.**

**Note: Mtume Paulo alilisema na yeye jambo hili kwa sababu heri hii aliipokea katika ufunuo mkubwa sana. *Filip 4: 10 – 13; Soma pia kwa makini Mdo. 3: 11 – 16, Mdo. 17: 28, (Maskini wa roho anafahamu daima kwamba bila Yesu yeye hawezi kufanya Jambo lolote.)***

III. **Heri walio maskini wa roho – Hii ni hali ya mwanafunzi kutototosheka ndani ya moyo wake na alivyoomba jana, au alivyotumika jana au alivyotoa jana, au alivyoimba na kusifu jana au alivyojitoa jana** n.k. yaani haridhiki ndani ya moyo wake kwamba ameshatumika vya kutosha au ametoa vya kutosha, au

ameomba vya kutosha la hasha, kila anapojilinganisha na maisha aliyoishi Yesu Kristo katika mwili alipokuwa hapa duniani anajikuta ni mdeni tu!! ***Filip 3: 12 – 14, 1kor 9: 26 – 27.***

- **Mwanafunzi aliye maskini wa roho ni yule ambaye wakati wake wote anamtaka Bwana na nguvu zake kumsaidia daima.** ***Zab 105: 4;*** Kumtaka Bwana Yesu ni hatua ya kwanza, lakini kutaka na nguvu zake ni hatua ya juu zaidi kwa mwanafunzi halisi wa Yesu Kristo. ***Kutoka 33: 12 – 23. (1Nyak 16: 11)***
- **Mafanikio ya Musa yalitokana na kuwa maskini wa Roho katika maisha yake yote, hakuwa ameridhika na miujiza aliyoishuhudia mbele ya Farao au katika bahari ya Shamu, au mana iliyoshuka jangwani n.k. daima alikuwa anahitaji atembee akiwa na ushirika wa karibu sana na Mungu.**
- Kumbuka tu kwamba Yesu Kristo wakati anawaaga wanafunzi wake na kuwabariki kabla ya kupaa kwenda kwa Baba yake baada ya kuwafundisha kwa maneno na kwa vitendo; ***Luk 24: 50 – 51.*** **Yesu hakuwapa wanafunzi wake magunia ya fedha wala dhahabu, bali aliwabariki na kuahidi kuwa nao siku zote na mahala pote watakapokwenda; na hii ikawa ndiyo siri ya ajabu na ya pekee sana ya mitume kufanya kazi ya Mungu iliyotukuka sana hadi makuhani wa dini nyingine wakaitii imani ya Mitume.** ***Mdo 6: 7***
- **Natamani leo kila mteule ajitambue kwamba yeye kama yeye hana uwezo wa kujitosheleza kiroho, na pia asitosheke na alivyoomba jana na juzi au alivyokwisha tumika huko nyuma; bali leo amtake Bwana na nguvu zake kwa upya ili apokee uwezo na neema ya kumvusha katika yote yaliyo mbele yake ambayo hayajui bado.** ***Amina***

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***July 2021***